ISSN 0856-6976

# MUHTASARI WA TAMKO LA SERA YA FEDHA

## *2023/24*

**GAVANA**

**BENKI KUU YA TANZANIA**

**Juni 2023**

ISSN 0856-6976

# MUHTASARI WA TAMKO LA SERA YA FEDHA

## 2023/24

**GAVANA**

**BENKI KUU YA TANZANIA**

**Juni 2023**

## Utangulizi

Kwa mujibu wa Sheria ya Benki Kuu ya Tanzania, Kifungu cha 21(3) hadi (6), Sura ya 197, Benki Kuu ya Tanzania inatakiwa kutoa Tamko la Sera ya Fedha mwezi Juni kila mwaka, likifuatiwa na tathmini ya nusu mwaka inayotolewa mwezi Februari. Tamko la Sera ya Fedha hutoa tathmini ya matokeo ya uandaaji na utekelezaji wa sera ya fedha, ikilinganishwa na malengo mapana ya Serikali na ya sera ya fedha ya kudhibiti mfumuko wa bei na kuchochea ukuaji wa uchumi. Kwa muktadha huu, tamko hili la Sera ya Fedha la Juni 2023 linajumuisha tathmini ya utekelezaji wa sera ya fedha kwa mwaka 2022/23, ikifuatiwa na mapitio ya mwenendo wa uchumi wa dunia na wa Tanzania. Vilevile, Tamko hili linatoa mwelekeo wa uchumi wa dunia na wa Tanzania na kuweka malengo ya sera ya fedha kwa mwaka 2023/24.

## Utekelezaji wa Malengo ya Sera ya Fedha ya Mwaka 2022/23

Katika kukabiliana na athari zilizotokana na misukosuko ya kiuchumi duniani, hususan athari za vita ya Ukraine na UVIKO-19, na kwa kuzingatia mwenendo wa uchumi wa Tanzania, mwaka 2022/23 Benki Kuu ilibadili mwelekeo wake wa utekelezaji wa sera ya fedha kwa kuanza kutekeleza sera ya fedha inayolenga kupunguza kasi ya ongezeko la ukwasi katika uchumi. Utekelezaji huu ulilenga kuhakikisha kuwa mfumuko wa bei unabakia ndani ya lengo la asilimia 5.4, na kuweka mazingira ya kuchochea ukuaji wa shughuli za kiuchumi na kudumisha uhimilivu wa sekta ya fedha. Ili kufikia malengo haya, Benki Kuu ililenga kutekeleza sera ya fedha yenye

malengo yafuatayo: (i) ukuaji wa fedha taslimu wa asilimia 11.4; (ii) ukuaji wa ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3) wa asilimia 10.3; (iii) ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi wa asilimia 10.7; na (iv) kuwa na akiba ya fedha za kigeni inayotosha kuagiza bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi kwa kipindi kisichopungua miezi minne. Aidha, malengo haya yanaendana na vigezo vilivyoainishwa katika programu ya Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) chini ya Mpango wa *Extended Credit Facility* (ECF).

Katika kufikia malengo hayo, Benki Kuu ilitumia nyenzo mbalimbali za sera ya fedha kwa ajili ya kusimamia kiwango cha ukwasi katika uchumi kulingana na mahitaji. Nyenzo hizo ni pamoja na kuingia mikataba ya mauziano ya dhamana kwa muda mfupi (*repurchase agreements*), kuuza dhamana za Serikali kwa ajili ya kupunguza ukwasi kwenye uchumi (*liquidity papers*) na kuuza fedha za kigeni katika soko la jumla la fedha za kigeni. Utekelezaji wa sera ya fedha ulifanikiwa kusimamia kiwango cha ukwasi katika sekta ya benki, kuendana na mahitaji ya shughuli mbalimbali za kiuchumi. Utekelezaji huu wa sera ya fedha ulisaidia pia kufikiwa kwa vigezo vilivyoainishwa katika programu kati ya Tanzania na Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) chini ya Mpango wa *Extended Credit Facility* (ECF) kwa mwaka 2022/23. Aidha, katika kipindi cha Julai 2022 hadi Aprili 2023, wastani wa fedha taslimu ulikua kwa asilimia 13.6, ikilinganishwa na lengo la asilimia 11.4 kwa mwaka 2022/23. Ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3) uliongezeka kwa wastani wa asilimia 12.8, ikilinganishwa na lengo la asilimia 10.3, hali inayoashiria ongezeko la shughuli za uchumi. Aidha, ukuaji wa

mikopo ya sekta binafsi uliimarika kwa kiwango kikubwa kufikia wastani wa asilimia 22.2, ikilinganishwa na lengo la asilimia 10.7, kwa mwaka 2022/23. Ukuaji huu unaakisi jitihada zinaoendelea kufanywa na Serikali katika kuboresha mazingira ya biashara na hivyo kusababisha ongezeko la mahitaji ya mikopo mipya kwa sekta binafsi, pamoja na sera wezeshi za fedha na bajeti. Vilevile, akiba ya fedha za kigeni ilibakia katika viwango vya kuridhisha kuweza kukidhi uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi kwa miezi 4.4, kiwango ambacho ni ndani ya lengo la nchi la kukidhi miezi isiyopungua minne.

**Mwenendo wa Uchumi wa Dunia**

Shughuli za kiuchumi duniani zilidorora mwaka 2022/23 kutokana na madhara ya vita inayoendelea nchini Ukraine, janga la UVIKO-19 na mabadiliko ya tabianchi. Vita ya Ukraine ilisababisha mvurugiko wa mnyororo wa ugavi ambao ulipelekea kuongezeka kwa bei za bidhaa katika soko la dunia na mfumuko wa bei. Aidha, maamuzi ya kupandisha riba za benki kuu katika nchi zilizoendelea kwa lengo la kukabiliana na mfumuko wa bei, yalisababisha hali ngumu ya kifedha katika soko la dunia na hivyo kuchangia ongezeko la gharama za mikopo kwa nchi zinazoendelea kiuchumi. Kutokana na mazingira haya, kasi ya ukuaji wa uchumi wa dunia inakadiriwa kupungua kwa mwaka 2022 ikilinganishwa na mwaka uliotangulia, huku matarajio ya ukuaji wa uchumi kwa mwaka 2023 yakiwa hafifu zaidi. Hata hivyo, kuanzia mwaka 2024 uchumi wa dunia unatarajiwa kuanza kuimarika kwa kasi ndogo, kutokana na matarajio ya kupungua kwa athari za misukosuko ya kiuchumi duniani.

Mfumuko wa bei duniani ulikuwa juu ya malengo katika nchi nyingi katika nusu ya kwanza ya 2022/23. Hali hii ilionekana zaidi katika nchi zilizoendelea. Aidha, mfumuko wa bei ulianza kupungua katika nusu ya pili ya mwaka kutokana na kupungua kwa bei za nishati na vyakula na matokeo ya utekelezaji thabiti wa sera ya fedha. Vilevile, mfumuko wa bei ulikuwa juu katika Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) ambapo nchi nyingi zilikuwa na mfumuko wa bei uliozidi vigezo vya mtangamano wa kiuchumi. Mfumuko wa bei unatarajiwa kupungua kuanzia nusu ya pili ya 2023/24 ukiakisi matokeo ya utekelezaji wa sera ya fedha inayolenga kupunguza ukwasi kwenye uchumi, pamoja na matarajio ya kupungua kwa bei za bidhaa katika soko la dunia.

Bei za bidhaa katika soko la dunia ziliongezeka mwaka 2022 kabla ya kuanza kupungua taratibu mwaka 2023. Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) linatarajia bei za bidhaa kuendelea kupungua katika siku zijazo. Hata hivyo, bei za bidhaa nyingi zimeendelea kuwa juu ya viwango vilivyokuwepo kabla ya kuibuka kwa vita nchini Ukraine. Bei ya dhahabu ilikuwa juu kutokana na ongezeko la mfumuko wa bei, kushuka thamani kwa dola ya Marekani na migogoro ya kisiasa inayoendelea. Kutokana na hali hii, benki kuu nyingi duniani zilinunua dhahabu kwa kiwango kikubwa kuliko kiasi kilichowahi kununuliwa katika miaka 55 iliyopita. Aidha, bei za mafuta ya petroli ziliongezeka japo zimeanza kupungua katika mwaka 2023 na zinatarajiwa kuendelea kupungua katika mwaka 2024, kutokana na matarajio ya kupungua kwa mahitaji katika soko la dunia. Hali hii itapunguza athari za maamuzi ya wanachama wa OPEC+ katika kupunguza kiwango cha uzalishaji wa mafuta ya petroli.

## Mwenendo wa Uchumi wa Tanzania

### Tanzania Bara

Mwenendo wa uchumi wa ndani ulikuwa wa kuridhisha mwaka 2022, licha ya changamoto zilizotokana na vita nchini Ukraine na athari za UVIKO-19. Mwenendo huu ulitokana na kuimarika kwa mchango wa sekta mbalimbali katika uchumi, hatua zilizochukuliwa na Serikali katika kuukinga uchumi dhidi ya athari za misukosuko ya kiuchumi duniani, uwekezaji unaoendelea kufanywa na Serikali na sekta binafsi, pamoja na hatua zinazochukuliwa na Serikali katika kuboresha mazingira ya biashara nchini. Uchumi wa Tanzania ulikua kwa asilimia 4.7 kwa mwaka 2022, ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 4.9 mwaka 2021. Shughuli zilizochangia ukuaji huu ni pamoja na kilimo, ujenzi na uchimbaji wa madini.

Kama ilivyo katika nchi nyingi duniani, mfumuko wa bei uliongezeka katika nusu ya kwanza ya 2022/23, kabla ya kuanza kupungua katika nusu ya pili. Ongezeko hili lilitokana na kupanda kwa bei za bidhaa katika soko la dunia, kupungua kwa upatikanaji wa chakula nchini kulikosababishwa zaidi na uhaba katika nchi za jirani na matarajio ya kupungua kwa uzalishaji kutokana na kuchelewa kwa mvua za vuli. Katika kipindi cha Julai 2022 hadi Aprili 2023, mfumuko wa bei ulifikia wastani wa asilimia 4.7, ikilinganishwa na asilimia 3.9 katika kipindi kama hicho mwaka 2021/22. Hata hivyo, mfumuko wa bei uliendelea kubakia ndani ya lengo la nchi la asilimia 5.4 kwa mwaka 2022/23, na vigezo vya mtangamano kwa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na Jumuiya ya Maendeleo

Kusini mwa Afrika (SADC). Aidha, mfumuko wa bei usiojumuisha bei za vyakula visivyochakatwa, nishati, na maji; ambao huchangia takriban asilimia 73.9 ya fahirisi za bei za bidhaa, ulikuwa asilimia 2.7 ikilinganishwa na asilimia 3.9 katika kipindi kama hicho mwaka 2021/22. Mfumuko wa bei unatarajiwa kuendelea kubaki ndani ya lengo kwa mwezi Mei na Juni 2023, na lengo la asilimia 5 kwa mwaka 2023/24.

Utekelezaji wa sera ya fedha uliolenga kupunguza ongezeko la ukwasi kwenye uchumi uliwezesha Benki Kuu kusimamia ukuaji wa ujazi wa fedha kulingana na malengo ya mwaka 2022/23. Ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3) ulikua kwa wastani wa asilimia 12.8, ikilinganishwa na wastani wa asilimia 13.1 katika kipindi kama hicho mwaka 2021/22 na lengo la ukuaji wa asilimia 10.3 kwa mwaka 2022/23. Ukuaji huu ulikuwa sambamba na mahitaji ya shughuli za kiuchumi. Wastani wa fedha taslimu ulikua kwa asilimia 13.6 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 13.9 katika kipindi kama hicho mwaka 2021/22 na lengo la ukuaji wa asilimia 11.4.

Mikopo kwa sekta binafsi ilikua kwa wastani wa asilimia 22.2 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 8.4 katika kipindi kama hicho mwaka 2021/22 na lengo la ukuaji wa asilimia 10.7. Ukuaji huu ulikuwa wa juu zaidi ikilinganishwa na viwango vya ukuaji katika nchi nyingine za Afrika Mashariki, hali iliyochangiwa zaidi na ongezeko la mahitaji ya mikopo mipya kufuatia jitihada zinazofanywa na Serikali katika kuboresha mazingira na sera za biashara, pamoja na utekelezaji wa sera wezeshi za fedha na za

bajeti. Mikopo iliyoelekezwa kwenye shughuli za kilimo ilikua kwa asilimia 36.1, ikiwa ni juu zaidi ya ukuaji wa mikopo iliyoelekezwa kwenye shughuli nyingine za kiuchumi. Ukuaji huu ulitokana na hatua zilizochukuliwa na Serikali ikiwa ni pamoja na kuongezeka kwa bajeti ya shughuli za kilimo, uwepo wa mkopo maalum wa shilingi trilioni moja kwa benki na taasisi za fedha kwa ajili ya kukopesha sekta ya kilimo, na unafuu wa kiwango cha kisheria cha amana ambacho benki na taasisi za fedha zinatakiwa kuweka Benki Kuu (SMR) kwa kutoa mikopo yenye riba nafuu kwa shughuli za kilimo nchini. Ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi unatarajiwa kuendelea kuwa imara kufuatia jitihada zinazoendelea kufanywa katika kuboresha mazingira ya biashara nchini pamoja na sera wezeshi za fedha na bajeti.

Kwa upande wa riba, katika kipindi cha Julai 2022 hadi Aprili 2023 riba ya siku moja katika soko la fedha baina ya mabenki ilikuwa ni ya wastani wa asilimia 3.54, ikilinganishwa na asilimia 3.42 katika kipindi kama hicho mwaka 2021/22. Riba zinazotozwa na mabenki kwa mikopo na zile za amana hazikuwa na mabadiliko makubwa. Wastani wa riba za mikopo ulibakia kuwa asilimia 16, wakati riba za amana zilibakia kuwa asilimia 7. Riba za mikopo inayotolewa kwa wateja wakubwa na wateja wenye sifa ya kulipa mikopo yao kwa wakati (*negotiated lending rates*) zilikuwa za wastani wa asilimia 13.91. Kasi ndogo ya kupungua kwa riba za mikopo inaashiria uwepo wa changamoto za kimfumo ambazo zimeshaanza kufanyiwa kazi na Serikali kupitia maboresho mbalimbali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa sekta ya fedha nchini.

Katika kipindi cha Julai 2022 hadi Aprili 2023, thamani ya shilingi ya Tanzania ilipungua kutokana na kuongezeka kwa mahitaji ya fedha za kigeni kwenye uchumi, kufuatia ongezeko la bei za bidhaa katika soko la dunia na kupungua kwa fedha za kigeni zinazoingia nchini kutokana na kupanda kwa riba ya sera ya fedha katika nchi zilizoendelea. Hata hivyo, kiwango cha kupungua kwa thamani ya shilingi kilikuwa chini ya asilimia moja kwa mwaka, kutokana na uwepo wa akiba ya kutosha ya fedha za kigeni na hatua zilizochukuliwa na Benki Kuu katika kuongeza utulivu sokoni na kuongeza umakini katika matumizi ya fedha za kigeni katika kipindi hiki chenye changamoto kadhaa duniani. Dola moja ya Marekani ilibadilishwa kwa wastani wa shilingi 2,319.80 ikilinganishwa na shilingi 2,308.87 katika kipindi kama hicho mwaka 2021/22.

Utekelezaji wa bajeti kwa kiwango kikubwa ulikuwa ndani ya malengo, licha ya changamoto kadhaa zilizotokana na misukosuko ya kiuchumi duniani. Katika kipindi cha Julai 2022 hadi Aprili 2023, makusanyo ya Serikali yalikuwa shilingi bilioni 21,666.2 sawa na asilimia 94 ya lengo. Kati ya hayo, mapato ya kodi yalikuwa shilingi bilioni 17,785.3, na shilingi bilioni 3,093.6 zilikuwa ni mapato yasiyo ya kodi. Matokeo haya yalichangiwa kwa kiasi kikubwa na kuimarika kwa shughuli mbalimbali za kiuchumi, kuboreshwa kwa hatua za usimamizi wa kodi na kuongezeka kwa ulipaji kodi kwa hiari. Matumizi ya Serikali yalikuwa shilingi bilioni 28,291.1, ambapo shilingi bilioni 16,290.1 zilikuwa ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na bakaa ilikuwa ni kwa matumizi ya miradi ya maendeleo. Deni

la Taifa la nje na ndani lilikuwa dola za Marekani milioni 41,222.7 mwishoni mwa mwezi Aprili 2023, kutoka dola za Marekani milioni 38,265.6 mwezi Juni 2022. Deni la umma (la nje na la ndani) lilikuwa dola za Marekani milioni 34,448.5, ikiwa ni ongezeko la dola milioni 3,556.9 kutoka kiwango kilichorekodiwa mwezi Juni 2022. Ongezeko hili lilitokana na mikopo mipya iliyochukuliwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Sekta ya nje iliendelea kukabiliwa na changamoto zinazotokana na athari za vita nchini Ukraine na UVIKO-19. Madhara ya changamoto hizi yamejitokeza kupitia ongezeko la bei za bidhaa katika soko la dunia, kuvurugika kwa minyororo ya ugavi, na kuongezeka kwa mfumuko wa bei katika nchi nyingi duniani. Aidha, changamoto hizi zimechangia kupungua kwa fedha za kigeni na thamani ya shilingi, pamoja na kuongezeka kwa gharama za kukopa katika masoko ya fedha kimataifa. Kutokana na changamoto hizi, nakisi ya urari wa biashara ya bidhaa, huduma na uhamishaji mali nchi za nje iliongezeka na kufikia dola za Marekani milioni 4,414.2 katika kipindi cha Julai 2022 hadi Aprili 2023, kutoka dola milioni 2,516.1 katika kipindi kama hicho mwaka 2021/22, kufuatia ongezeko la thamani ya bidhaa na huduma zilizoagizwa kutoka nje ya nchi, ikilinganishwa na thamani ya bidhaa na huduma zilizouzwa nje ya nchi. Akiba ya fedha za kigeni ilipungua na kufikia dola za Marekani milioni 4,881.2 mwishoni mwa mwezi April 2023, ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 5,461.4 mwezi Aprili 2022. Kiwango hiki kinatosheleza uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi kwa takriban miezi 4.4, kiwango ambacho ni ndani ya lengo la nchi

la kukidhi miezi isiyopungua minne.

Katika kipindi cha Julai 2022 hadi Aprili 2023, mauzo ya bidhaa na huduma nje ya nchi yaliongezeka kwa asilimia 15.7 hadi dola za Marekani milioni 10,561.6, kufuatia ongezeko la mapato ya usafirishaji, madini na bidhaa za viwandani. Mapato yatokanayo na huduma yaliongezeka kwa asilimia 39.6 kufikia dola za Marekani milioni 4,441.4, kutokana na kuongezeka kwa mapato ya utalii na usafirishaji. Wakati huohuo, thamani ya bidhaa na huduma zilizoagizwa kutoka nje ya nchi iliongezeka kwa asilimia 30 kufikia dola za Marekani milioni 14,428.5 kutokana na kuongezeka kwa thamani ya bidhaa za mafuta ya nishati kufuatia kupanda kwa bei katika soko la dunia. Kutokana na mwenendo huu, nakisi ya urari wa biashara ya bidhaa, huduma na uhamishaji mali nchi za nje inakadiriwa kufikia asilimia 5 ya Pato la Taifa kwa mwaka 2022/23, ikilinganishwa na asilimia 4.6 mwaka 2021/22. Aidha, nakisi hii inatarajiwa kupungua na kufikia asilimia 4 ya Pato la Taifa katika kipingi cha miaka mitatu hadi mitano ijayo.

Sekta ya benki imeendelea kuimarika ambapo katika kipindi cha mwezi Julai 2022 hadi Aprili 2023, sekta hiyo ilikuwa na kiwango cha kutosha cha mitaji na ukwasi, na iliendelea kutengeneza faida, na hivyo kuchangia katika utekelezaji thabiti wa sera ya fedha. Sekta iliendelea kunufaika na matumizi ya teknolojia katika utoaji wa huduma, hali iliyochangia ongezeko la amana na rasimali, huku ikiendelea kuhimili misukosuko ya kiuchumi ya ndani na nje ya nchi. Ubora wa rasilimali umeendelea kuimarika, ambapo mikopo

chechefu ilipungua hadi wastani wa asilimia 5.5 ya mikopo yote mwezi Aprili 2023, kutoka asilimia 7.8 mwezi Juni 2022. Aidha, uwiano huu unakaribia kiwango kinachokubalika na Benki Kuu cha asilimia 5. Kupungua kwa mikopo chechefu kunatarajiwa kuchochea ongezeko la mikopo yenye riba nafuu kwa sekta binafsi. Benki Kuu imeendelea kuchukua hatua kwa lengo la kuhakikisha mikopo chechefu inaendelea kupungua. Hatua hizo ni pamoja na kuzitaka benki na taasisi za fedha kuzingatia vihatarishi vyote wakati wa kuidhinisha mikopo na kufuatilia benki na taasisi za fedha kuhakikisha kuwa zinatekeleza mikakati yao kwa ajili ya kupunguza mikopo chechefu. Hatua nyingine ni kusisitiza matumizi ya kanzidata ya taarifa za wakopaji katika kuidhinisha mikopo mipya na kuzitaka benki kuwasilisha taarifa za mikopo kwenye kanzidata ya taarifa za wakopaji. Vilevile, Benki Kuu inaendelea kuhimiza wafanyakazi wa benki kufuata maadili na miongozo ya kiutendaji iliyoainishwa na Jumuiya ya Mabenki Tanzania (TBA).

Mifumo ya malipo imeendelea kufanya kazi kwa ufanisi mwaka 2022/23 na hivyo kurahisisha utekelezaji wa sera ya fedha na kufanikisha shughuli za kiuchumi nchini. Matumizi ya simu za mkononi ambayo idadi ya watumiaji wake ilifikia milioni 61.8 mwezi Aprili 2023, yameendelea kuwezesha wananchi wengi kufikiwa na huduma za kifedha kwa gharama nafuu. Idadi ya watu wazima waliofikiwa na huduma za fedha kupitia simu zao za mikononi ilifikia asilimia 86 mwezi Aprili 2023, ikilinganishwa na asilimia 79 katika kipindi kama hicho mwaka 2021/22. Aidha, Benki Kuu imeendelea kutekeleza mradi wa mfumo wa malipo ya papo kwa hapo (TIPS),

ambao unalenga kuongeza muingiliano baina ya watoa huduma za fedha nchini. Hadi kufikia Aprili 2023, watoa huduma za kifedha 40 walikuwa wameunganishwa na mfumo huu wa TIPS, ikilinganishwa na watoa huduma 34 waliokuwepo mwaka 2021/22. Aidha, idadi na thamani ya miamala kwenye mfumo huu imeendelea kuongezeka kwa kasi ya kuridhisha.

**Zanzibar**

Uchumi wa Zanzibar ulikuwa imara mwaka 2022, ukikua kwa asilimia 6.8, ikilinganishwa na makadirio ya ukuaji wa asilimia 5.4, na ukuaji wa asilimia 5.1 mwaka 2021. Ukuaji huu ulitokana na kuimarika kwa shughuli mbalimbali za kiuchumi, hususan huduma za utalii, mifugo, ujenzi, viwanda na upangishaji majengo.

Mfumuko wa bei ulikuwa wastani wa asilimia 7.1 katika kipindi cha Julai 2022 hadi Aprili 2023, ikilinganishwa na asilimia 2.7 katika kipindi kama hicho mwaka 2021/22. Ongezeko hili lilichangiwa na kupanda kwa bei za vyakula na bidhaa zisizo za chakula katika soko la dunia kutokana na athari ya vita nchini Ukraine. Mfumuko wa bei unatarajiwa kubaki ndani ya tarakimu moja katika kipindi kilichosalia cha mwaka 2022/23 na 2023/24, kutokana na matarajio ya kupungua kwa bei za nishati na vyakula katika soko la dunia.
Mapato ya Serikali, yanayojumuisha mapato ya ndani na misaada yaliongezeka kwa aslimia 32.1 kufikia shilingi bilioni 1,043.9, kutoka shilingi bilioni 790.1 katika kipindi kama hicho mwaka 2021/22. Mapato ya kodi yalikuwa shilingi bilioni 872.1, sawa na asilimia 94.9

ya lengo. Mapato yasiyo ya kodi yalikuwa shilingi bilioni 132, sawa na asilimia 83.6 ya lengo. Matumizi ya Serikali yalikuwa shilingi bilioni 1,149.1, ambapo kati ya hizo matumizi ya kawaida yalikuwa shilingi bilioni 801.9, na matumizi ya maendeleo yalikuwa shilingi bilioni 347.1. Deni la Serikali liliongezeka na kufikia shilingi bilioni 2,742.6 mwezi Aprili 2023, kutoka shilingi bilioni 1,224.4 mwishoni mwa mwezi Juni 2022. Ongezeko hili kwa kiasi kikubwa lilitokana na marekebisho yaliyoambatana na uhakiki wa takwimu za madeni, na mikopo mipya.

Urari wa biashara ya bidhaa, huduma na uhamishaji mali nchi za nje ulikuwa na nakisi ya dola milioni 286.7 katika kipindi cha Julai 2022 hadi Aprili 2023, ikilinganishwa na nakisi ya dola za Marekani milioni 208.8 katika kipindi kama hicho mwaka 2021/22. Mwenendo huu ulichangiwa na kuongezeka kwa bei za bidhaa katika soko la dunia. Mapato yatokanayo na mauzo ya bidhaa na huduma nje ya nchi yalifikia dola za Marekani milioni 186, kutoka dola milioni 157.7, hali iliyosababishwa na kuongezeka kwa mapato yatokanayo na shughuli za utalii. Mapato yatokanayo na uuzaji wa huduma nje ya nchi yaliongezeka kwa asilimia 71.8, hadi dola za Marekani milioni 124.5, kutokana na kuimarika kwa sekta ya huduma. Thamani ya bidhaa na huduma zilizoagizwa kutoka nje ya nchi iliongezeka kwa asilimia 31.9, hadi dola za Marekani milioni 501.2 katika kipindi cha Julai 2022 hadi Aprili 2023. Ongezeko hili kwa kiwango kikubwa lilitokana na uagizaji wa mafuta ya nishati, bidhaa za chakula, mashine, na vifaa vya ujenzi.

## Matarajio ya Uchumi na Malengo ya Sera ya Fedha ya Mwaka 2023/24

Malengo ya kiuchumi ya Serikali yanaongozwa na Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 - 2025/26 (FYDP III) na Mpango wa Maendeleo wa Zanzibar (ZADEP). Malengo haya ya kiuchumi yamezingatia pia athari zitokanazo na misukosuko ya kiuchumi duniani, kama vile mfumuko wa bei, kupanda kwa riba za sera ya fedha, na hali ngumu ya kifedha duniani. Kwa muktadha huu, malengo ya kiuchumi ya mwaka 2023/24 ni kama ifuatavyo:

i. ukuaji halisi wa Pato la Taifa wa asilimia 5.2 kwa mwaka 2023 na asilimia 6.1 kwa mwaka 2024 kwa Tanzania Bara; na ukuaji wa asilimia 7.1 mwaka 2023 na asilimia 7.4 mwaka 2024 kwa uchumi wa Zanzibar; na
ii. mfumuko wa bei unatarajiwa kubakia ndani ya wastani wa asilimia 5 mwaka 2023/24, kwa Tanzania Bara na Zanzibar.

Kutokana na matarajio ya mwenendo wa hali ya uchumi wa dunia na uchumi wa Tanzania, Benki Kuu itaendelea kutekeleza sera ya fedha inayolenga kupunguza ongezeko la ukwasi katika uchumi kwa mwaka 2023/24. Hatua hii inalenga kuhakikisha kuwa malengo ya mfumuko wa bei yanatimizwa na kuendelea kuchochea kuimarika kwa shughuli za kiuchumi nchini. Aidha, utekelezaji wa sera ya fedha kwa nusu ya kwanza ya mwaka 2023/24 utafanyika kwa kutumia mfumo wa sasa unaolenga kusimamia ujazi wa fedha katika kufikia malengo mapana ya kiuchumi. Malengo ya sera ya fedha chini ya mfumo huu yatakuwa kama ifuatavyo:

i. ukuaji wa fedha taslimu wa asilimia 10.1;
ii. ukuaji wa ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3) wa asilimia 10.1; na
iii. ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi wa asilimia 16.4.

Utekelezaji huu wa sera ya fedha unalenga pia kufikiwa kwa vigezo vilivyoainishwa katika makubaliano na Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) chini ya Mpango wa *Extended Credit Facility (ECF*).

Katika nusu ya pili ya mwaka 2023/24, utekelezaji wa sera utaongozwa na mfumo wa sera ya fedha unaotumia riba ya Benki Kuu katika kusimamia malengo mapana ya kiuchumi. Mfumo huu unalenga kuboresha utekelezaji wa sera ya fedha katika kudhibiti mfumuko wa bei na kuchangia ukuaji wa uchumi.

Malengo ya sera ya fedha kwa nusu ya pili ya mwaka 2023/24 chini ya mfumo mpya yataainishwa katika mapitio ya nusu mwaka ya Tamko la sera ya fedha, ambalo litatolewa mwezi Februari 2024. Maelezo ya kina kuhusu mfumo wa sera ya fedha unaotumia riba yameainishwa kwenye Mwongozo wa Mfumo wa Sera ya Fedha wa mwaka 2023.

Katika mifumo yote miwili Benki Kuu itaendelea kuhakikisha uwepo wa akiba ya fedha za kigeni inayotosha kuagiza bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi kwa kipindi kisichopungua miezi minne. Benki Kuu itaendelea pia kufuatilia kwa karibu maendeleo ya uchumi wa dunia na wa Tanzania kwa lengo la kuchukua hatua za ziada pale

itakapohitajika ili kuhakikisha mfumuko wa bei unabaki ndani ya lengo, na kuendelea kuchochea ukuaji wa shughuli za kiuchumi na kudumisha uhimilivu wa sekta za kifedha.

Aidha, katika jitihada za kuhakikisha kwamba mabadiliko ya mfumo wa utekelezaji wa sera ya fedha yanafanyika kwa ufanisi na kuanza kutekelezwa mwezi Januari 2024, Benki Kuu itaendelea kufanya maboresho katika mfumo wa modeli za kiuchumi na kuongeza uwezo katika kufanya makadirio ya viashiria mbalimbali vya kiuchumi, ikiwa ni pamoja na kushirikisha wadau mbalimbali kwa ajili ya kuboresha na kuhakikisha kunakuwepo na upatikanaji na wa takwimu bora kwa wakati. Aidha, Benki Kuu itaendelea kutoa elimu kwa wadau juu ya mfumo huu wa sera ya fedha na kuboresha miundombinu ya soko la fedha ili kuongeza ufanisi kwa lengo la kurahisisha upatikanaji na ubadilishanaji wa ukwasi baina ya mabenki.

## Hitimisho

Shughuli za kiuchumi duniani zilidorora mwaka 2022 na hali hii inatarajiwa kuendelea kwa sehemu kubwa ya mwaka 2023/24. Hii inatokana na athari za vita ya Ukraine na changamoto za hali ya hewa. Mfumuko wa bei ulikuwa juu ingawa unatarajiwa kupungua, sambamba na kupungua kwa bei za bidhaa katika soko la dunia, hususan bei za vyakula na nishati, na matokeo ya sera ya fedha inayolenga kupunguza ukwasi kwenye uchumi.

Kwa kuzingatia mwenendo wa uchumi wa dunia, hatua za kisera na utekelezaji wa programu zenye lengo la kuchochea uzalishaji zilizochukuliwa na Serikali hapa nchini katika kukabiliana na misukosuko ya kiuchumi, shughuli za kiuchumi zinatarajiwa kuimarika kuanzia mwaka 2023 na kuendelea. Uchumi waTanzania Bara na Zanzibar unatarajiwa kukua kwa asilimia 5.2 na asilimia 7.1 mwaka 2023, mtawalia. Mfumuko wa bei unatarajiwa kuwa ndani ya lengo la asilimia 5 kutokana na matarajio ya kuendelea kupungua kwa bei za bidhaa katika soko la dunia na upatikanaji wa chakula cha kutosha.

Kwa muktadha huo, katika mwaka 2023/24, Benki Kuu itaendelea kutekeleza sera ya fedha inayolenga kupunguza ongezeko la ukwasi, ili kufanikisha lengo la utulivu wa mfumuko wa bei, kuchochea kuimarika kwa shughuli za kiuchumi, na kudumisha uhimilivu wa sekta ya fedha. Utekelezaji wa sera ya fedha kwa nusu ya kwanza ya mwaka 2023/24 utafanyika kwa kutumia mfumo wa sasa unaolenga kusimamia ujazi wa fedha ili kufikia malengo

mapana ya kiuchumi, wakati katika nusu ya pili utekelezaji wa sera ya fedha utaongozwa na mfumo wa sera ya fedha unaotumia riba ya Benki Kuu. Benki Kuu itaendelea kufuatilia kwa karibu viashiria mbalimbali vya kiuchumi na kuchukua hatua za ziada pale itakapobidi. Kwa muktadha huu, Benki Kuu ya Tanzania ina matumaini kuwa malengo yaliyoainishwa katika Tamko hili la Sera ya Fedha ya mwaka 2023/24 yatafikiwa.

Kwa maelezo zaidi wasiliana na:
Mkurugenzi wa Utafiti na Sera za Uchumi
Benki Kuu ya Tanzania, 16 Barabara ya Jakaya Kikwete 40184,
S. L. P 2302, Dodoma, Tanzania
Barua pepe: botcommunications@bot.go.tz
Tovuti: https://www.bot.go.tz